



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA

BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)



## TANGAZO

### MALIPO YA ADA ZA MWAKA (RETENTION FEE) KWA NJIA YA MTANDAO

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwatangazia Wataalam wote ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada wenye Usajili wa kudumu (Enrollment & Full Registration) kuwa

1. Malipo ya ada za mwaka ni takwa la kisheria hivyo kila Mtaalam anatakiwa kulipia ada ya mwaka kwa wakati ili aruhusiwe kufanya kazi za kitaaluma.
2. Ada za mwaka zinalipwa kwa kufuata mwaka wa fedha wa Serikali ambao unaanza kila tarehe 01 Julai ya mwaka husika na kuisha tarehe 30 Juni ya mwaka unaofuata.
3. Malipo ya ada za mwaka yanafanyika kwenye mfumo wa usajili wa HPRS ([hprs.moh.go.tz](http://hprs.moh.go.tz)) katika kipengele cha **LICENSING** na kuomba control namba katika kipengele cha **PAYMENT**
4. Malipo ya Usajili na ada za mwaka yanafanyika kupitia Control namba kwa njia ya **benki / Wakala wa benki ya NMB** au kwa njia ya **Simu malipo ya Serikali**
5. Kwa Wataalam waliopata usajili wa kudumu na bado hawajatengenezewa akaunti za mfumo wa Usajili wa HPRS wawasiliane na ofisi ya Msajili ndani ya masaa ya kazi ili wapatiwe huduma
6. Mtaalam ambaye atakuwa na malimbikizo ya madeni ya ada za mwaka hataweza kutengenezewa akaunti ya mfumo mpaka amelipia madeni yake yote.
7. Wataalam wote watapaswa kuingiza taarifa zao kwenye mfumo ili waendeleo kutambulika na Baraza kwa mujibu wa Sheria

Mawasiliano Simu: 0734005777, Email: [hlpc@afya.go.tz](mailto:hlpc@afya.go.tz)

Imetolewa na ofisi ya Msajili  
Baraza la Wataalam wa Maabara

